JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI**

# UENDESHAJI NA MATENGENEZO MIRADI YA MAJI

**MACHI, 2017**

**UENDESHAJI NA MATENGENEZO MIRADI YA MAJI**

YALIYOMO

- Ufahamu kwa Ujumla
- Miradi ya kusukuma na Mashine
- Miradi ya Mserereko
- Visima vifupi na Pampu za Mkono
- Mashine (Generator)

**Ufahamu kwa Ujumla**

**Lengo Kuu:**

Kujenga uelewa sahihi wa Uendeshaji na Matengenezo kwa COWSOs na Jamii

**Malengo Mahususi**

- Maana ya Undeshaji na matengezo
- Aina za matengenezo
- Kutofautisha Uendeshaji na Matengenezo kwa aina mbalimbali za miradi

**UENDESHAJI NA UTENGENEZAJI**

**Maana ya Uendeshaji**

Ni hali ya kuangalia shughuli nzima ya mashine na eneo husika kwa ujumla kuanzia mashine inapoanza kufanya kazi mpaka pale inaposimamishwa kazi.

**Maana ya matengenezo**

Ni hali ya kufanya zoezi zima la mashine kuendelea kufanya kazi bila tatizo lolote.

**Aina za matengenezo**

**Matengenezo ya kuzuia:**

- Unaofanywa wakati mfumo upo katika uendeshaji
- Uliopangwa kufanyika katika kipindi maalum
- Kubadilishwa kwa vipuli kabla ya kuisha kabisa muda wake
- Inausihwa kuweka machine katika hali nzuri bila ya kutegemea mabadiliko/matengenezo


**Matengezo ya dharura:**


- Ni matengezo ambao yanafanyika kwa ajili ya kuboresha au kubadilisha kifaa kilichoshindwa kufanya kazi au kuharibika

**Uendeshaji na Matengenezo katika mradi wa maji wa mserereko**

Uendeshaji wa mradi wa maji ya mserereko unahusu kuangalia mwenendo mzima wa mradi unavyofanya kazi ikiwa ni pamoja na.

- kunakili kiwango cha mita wakati unaanza kufungua maji na kiwango mita wakati unafunga maji
- taarifa ya tatizo lolote linalotokea katika mradi huo wa maji,
- Kiasi cha pesa kinachoingia na kutoka
- Kufamnya matengenezo kwenye miundombinu kwa mfano; tanki la maji, sehemu ya chanzo, njia za mabomba, mita ya maji, sehemu za kuchotea maji nk.
- **Angalizo:** matatizo yote huwa yanatatuliwa pale pale au yanawekewa ratiba.




Stream source
Catchment
Intake
Sedimentation tank
Break pressure tank
Inlet pipe
Outlet pipe
Distribution chamber
Branch line
Reservoir
Reservoir tank
Valve box
Tap
Tap stand
Tap stand
Distribution line
Sub-system
Sub-system

**Matengenezo ya mradi mserereko**

| Tatizo | Sababu ya tatizo | Matengenezo |
|---|---|---|
| Bomba linapasuka mara kwa mara | • Bomba imelazwa katika kina kifupi<br>• Bomba linaubora mdogo | Badilisha kipande cha bomba weka chenye ubora unatakiwa, Ongeza kina cha kulaza bomba |
| Maji hayatoki bombani | • Bomba limepasuka<br>• Koki zimefungwa<br>• Maji yameisha kwenye tanki<br>• Bomba limezibwa | • Unga au ziba mahali bomba lilipopasuka<br>• Koki zifunguliwe<br>• Jaza Maji kwenye tanki<br>• Zibua mahali bomba lilipozibwa |
| Maji sio masafi | • Maji yamechafuliwa kwenye chanzo<br>• Maji yamechafuka kutokana na bomba kupasuka | • Angalia mbinu sahihi ya kutibu maji kulingana na aina ya uchafu ulioingia |
| Nguvu ya msukumo wa maji ni ndogo | • kutokana na bomba kupasuka<br>• Hewa imeigia kwenye bomba | • Unga au ziba mahali bomba lilipopasuka<br>• Fungua air valve |

Jinsi ya kujaza kumbukumbu ya matengenezo ya mradi wa maji ya mserereko


| Tarehe | Tatizo | Sababu ya tatizo | Utatuzi wa tatizo | Imetengenezwa | Vipuli vilivyotumika | Gharama |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 26.6.2015 | Maji yanatoka kidogo kwenye kituo | Bomba linavuja | Kuunga kipande kingine cha bomba | Ally | Kipande cha bomba 4” | 5000/= |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

**Uendeshaji na matengenezo wa pampu ya mkono**

Uendeshaji wa pampu ya mkono unahusisha mwenendo mzima wa matumizi ya pampu kuanzia pampu inapoanza kazi mpaka inaposimamishwa.

Kuna aina mbalimbali za pampu ya mkono zinazotumika vijijini ambazo ni

- Afridev hand pump
- India MK II hand pump
- Nira AF (76,84,850
- Tara Handpump
- Bucket Pumps
- Monolift



Pump rod
Outlet
Cylinder
Piston
Piston valve
Foot valve
Suction lift
Rising main



Watu wakichota maji kwenye kisima kinachotumia pampu ya mkono

**Matengenezo ya pampu ya mkono**

Matengenezo ya pampu ya mkono yamegawanyika katika sehemu mbili

- Matengenezo ya dharura
- Matengenezo ya kuzuia
- Matengenezo ya dharura yanafanyika kila wakati pale pampu inapokua na matatizo.


Pampu ya mkono ni kama vifaa vingine vya mekaniko vinavyohitaji matengenezo kuifanya iendelee kuwa katika hali nzuri. Ukiondoa matengenezo ya kuzuia, matengenezo ya dharura ya pampu ya mkono yanaweza kutokea na kusababisha matatizo katika mladi wa maji ya pampu ya mkono. Njia zinazohusisha matengenezo ni:

- Kuelewa sababu,matatizo na hatua za kuchukua

- Kutenganisha pampu kama inahitajika,
- Kuunganisha pampu baada ya kuondoa vitu vilivyoharibika,
- Kuweka taarifa za kumbukumbu kwa ajili ya matengenezo

**Jedwali hapo chini linaonyesha mfano wa matatizo yanayoweza kutokea kwenye pampu ya mkono**

| TATIZO | KIASHIRIA | SABABU | MATENGENEZO |
| --- | --- | --- | --- |
| Mkono wa pampu unacheza | • Kichwa kinatingishika<br>• Stendi ya pampu haijashika vizuri | •Fulcrum bushes zimesagika<br>•Pini imetoka<br>•Boliti zimelegea | •Badilisha bushi<br>•Weka pini nyingine<br>•Kaza boliti |
| Sauti zisizo za kawaida | • Mkono wa pampu haupo vizuri | Bushi zimesagika<br>Mkono unagusa kichwa cha pampu | Badilisha bushi<br>Badilisha benti na rodi |
| Maji hayatoki | Mkono wa pampu unakwenda bila kusukuma hewa. | Mkono wa pampu haujaunganishwa<br>Bomba la kuvuta maji limetengana na pampu<br>Kina cha maji kimeshuka chini | Unganisha mkono wa pampu na bomba la kuvuta maji<br>Pima kina cha ,maji ili uangalie mahali mahali ilipo pampu kama ipo kwenye maji |



Fomu ya matengenezo ya pampu ya mkono

| Tarehe | Tatizo | Sababu ya tatizo | Utatuzi wa tatizo | Imetengenezwa | Vipuli vilivyotumika | Gharama |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 26.6.2015 | Mkono wa Pampu umelegea | Pini ya mkono imekatika | Kubadilishwa kwa pini na kuwekwa nyinge | Ally | Pini ya Mkono | 15000/= |

**Sahihi ya msimamizi**……………………….

**Sahihi ya fundi**……………………..

**Uendeshaji na matengenezo ya jenereta**

**Jenereta** ni mashine ambayo inabadili nishati ya mekaniko na kuwa nishati ya umeme.

Miradi ya maji vijijini mingi inatumia Jenereta kwa ajili ya kuzalisha umeme ambao unatumika kwenye pampu za kusuma maji. Jenereta zinahitaji uendeshaji na matengenezo wakati wote wa matumizi yake.

**Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uendeshaji na matengenezo ya jenereta**

**Kanuni za usalama kwa ujumla:**


- Vaa buti ngumu
- Weka sehemu ya jenereta iwe kavu ili kuzuia kutereza na kupata kutu
- Vaa nguo zinazoshika mwili.
- Usininginize kitu chochote kama vitu vya kusafishia au vitendea kazi kwenye nguo ya kufanyia kazi

**Uendeshaji wa jenereta wakati wote**

- Fungua madirisha na hakikisha genereta linapata hewa ya kutosha
- Usifungue milango ya radieta
- Weka vidole mbali na vitu vinavyozunguka
- Hakikisha wakati wote sakafu ni kavu na usafi wa eneo husika

**Wakati wa matengenezo**

- Usifanye marekebisho yeyote ya kitu usichokielewa
- Matengenezo yafanyike wakati injini imezimwa na mwanga wa kutosha
- Hakikisha betri haijaunganishwa wakati unafanya marekebisho




**PICHA YA JENERETA INAYOTUMIKA KUZALISHA NISHATI ILI KUVUTA NA KUSUKUMA MAJI.**

# Fomu ya msimamizi wa jenereta:

| tarehe | kuanzia | | Kipindi cha uendeshaji | | mwisho | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Fuel added(litre) | Start time | Voltage(volts) | Current(amps) | time | Kw-hrs(metre-reading) | Water pumped(meter reading) | Maelezo ya matatizo aliyoyaona | Jina la muangaliz |
| | | | | | | | | | |

**Saini ya Pampu Opareta…………………………………….**

**Saini ya Fundi………………………………………………….**

**Tarehe…………………………………………………………**

**FOMU YA KUJAZA MATENGENEZO YALIYOFANYIKA**

| **KIPENGELE** | **SEHEMU** | **CHECKED(tick if checked)(weka alama kama imekaguliwa)** | **WORKDONE (kazi iliyofanyika)** | **COMMENTS (maelezo)** |
|---|---|---|---|---|
| VILAINISHI (LUBRICANT) | *Engine oil* (mafuta ya injini) | | | |
| | *Oil filter* (mafuta ya filta) | | | |
| | Greasing (grisi) | | | |
| FUEL SYSTEM (MFUMO WA MAFUTA) | *Fuel filter* (kichuja mafuta) | | | |
| | *Injection/fuel pump (leakages)* | | | |
| | *Fuel lines(cracks, leaks)* | | | |
| ENGINE(INJINI) | Belts, air filter, plug/injectors | | | |
| ELECTRICAL(UMEME) | Battery | | | |